

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)**

**MALALAMIKO NAMBA. GA.71/135/335**

**SADIKI JUMA MCHAKULA.....MLALAMIKAJI  
DHIDI YA**

**SHIRIKA LA UGAVI WA UMEME NCHINI (TANESCO).....MLALAMIKIWA**

---

**TUZO YA MAKUBALIANO**

---

*(Imetolewa na Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kupitia waraka wake namba 19  
wa tarehe 15 Oktoba, 2021)*

**1.0 Maelezo ya Awali**

Mnamo tarehe 27 Aprili 2021, Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bw. Sadiki Juma Mchakula wa Mtaa wa Katubuka, Kata ya Katubuka, Manispaa ya Kigoma-Ujiji, Mkoa wa Kigoma dhidi ya Shirika la Umeme Tanzania ("TANESCO") (Mlalamikiwa). Mlalamikaji analalamikia kitendo cha Mlalamikiwa kumbadilisha kutoka daraja la watumiaji wadogo D1 na kumpeleka kwenye daraja la watumiaji wa kati T1 ilihali matumizi ya Mlalamikaji yako chini ya uniti 75 kwa mwezi.

Mlalamikaji ambaye dira yake ni namba 43000694281 anaeleza kwamba Mlalamikiwa alimhamisha kutoka kundi la watumiaji wadogo D1 hadi kwenye kundi la watumiaji wa kati T1 bila taarifa yeyote. Mlalamikaji anaendelea kueleza kuwa mwanzoni alikua akinunua umeme kwa shilingi TZS 9000 anapata uniti

73.8 lakini sasa hivi akinunua umeme kwa shilingi TZS 10,000 anapata uniti 28. Mlalamikaji hakuelewa kwa nini imekua hivyo ilihali matumizi yake ni wastani wa uniti 55 kwa mwezi. Hivyo basi, Mlalamikaji ameleta malalamiko yake EWURA na kuiomba Mamlaka imuamuru Mlalamikiwa kumrejsha kwenye kundi la watumiaji wadogo wa umeme D1.

Baada ya kupokea malalamiko ya Bw. Sadiki Juma Mchakula, Mamlaka (EWURA) tarehe 3 Mei 2021 ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuwasilisha utetezi kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (1) cha Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro '*Rule 6 (1) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Complaints Handling Procedure) Rules, GN No. 428/2020*'.

Mnamo tarehe 24 Juni 2021 Mlalamikiwa alileta utetezi wake na kuiambia Mamlaka yafuatayo;

- a) kwamba Mlalamikiwa anakiri kupokea malalamiko ya Mlalamikaji na kuyaelewa,
- b) kwamba Mlalamikaji ni mteja wa Mlalamikiwa na matumizi yake ya umeme ni ya daraja (tarrif) T1,
- c) kwamba madai ya Mlalamikaji kwamba anastahili kuwekwa katika daraja (tarrif) D1 si ya kweli kwa kuwa hajakidhi vigezo vilivyoainishwa kwa yeye kuwa katika daraja D1,
- d) kwamba Mlalamikiwa alishamfafanulia Mlalamikaji juu ya madai ya Mlalamikaji kupitia barua ya tarehe 15/4/2021 ambayo imeambatanishwa katika utetezi huu kama kielelezo T1; na
- e) kwamba Mlalamikaji analipia umeme katika daraja sahihi kabisa kulingana na vigezo vilivyowekwa na sheria.

Vikao vya usuluhishi baina ya pande zote mbili vilifanyika tarehe 1 Julai 2021 na tarehe 8 Septemba 2021 katika ukumbi wa mikutano Greenview Hoteli katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, mkoa wa Kigoma. Mwisho wa kikao cha usuluhishi pande zote mbili zilikubaliana kwamba Mlalamikiwa atamrejsha Mlalamikaji kwenye kundi la watumiaji wadogo la D1 kabla ya tarehe 10 Septemba 2021.

Makubaliano haya yamefupishwa kimaandishi kama inavyoainishwa kwenye 'Rule 14 (4) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Complaints Handling Procedure) Rules, GN. No 428/2020' na kama inavyoainishwa kwenye fomu ya makubaliano.

**2.0 Makubaliano:**

Pande zote mbili zimefikia muafaka na kwa mujibu wa Kanuni ya 14 ' Rule 14 (5) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Complaints Handling Procedure) Rules, GN. No 428 of 2020', makubaliano haya yameandikishwa kama Tuzo ya Mamlaka. Kila pande itabeba gharama zake katika shauri hili.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji-EWURA Dodoma tarehe 15 Oktoba, 2021.



.....  
**KAPWETE LEAH JOHN**  
**KATIBU WA BODI**